JINA.....NAMABARI.....

SHULE.....TAREHE.....

DARASA.....SAHIHI.....

102/3
KISWAHILI
MUDA: SAA 2½
KARATASI YA TATU (FASIHI)

KCSE ACHIEVERS PREDICTION

Hati ya kihitimu Elimu ya Sekondari Nchini Kenya (K.C.S.E)

KIDATO CHA NNE

MAAGIZO

a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu
b) Jibu maswali manne pekee
c) Swali la kwanza ni la lazima
d) Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobakia yaani : Riwaya, hadithi fupi,ushairi na fasihi simulizi
e) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja
f) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili
g) Majibu yote sharti yaandikwe kwenye nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SWALI	UPEO	ALAMA
USHAIRI	20	
TAMTHILIA	20	
RIWAYA	20	
HADITHI FUPI	20	
FASIHI SIMULIZI	20	
JUMLA		

©The Kenya National Examinations Council
Contact 0724333200/ 0795491185/ 0768321553 Marking Scheme

SEHEMU A : USHAIRI

1. **Lazima**

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

Lipi la kutenda, kwa walimwengu, liwe jema?
Liwe ni kupenda, bila uchungu, na lawana,
Niwe kama punda, pasipo fungu, wala kima.

Lipi liso inda, kwa walimwengu, na lazima?
Liwe la kuonda, kukupa Mungu, lisokwama,
Laiti si winda, enyi nduzangu, lau kama.

Kipi cha kupanda, kwa walimwengu, cha salama?
Kiwe kama tunda, au furungu, la mtama,
Hata zao nyonda, siunge zangu, na kuvama.
Ni wapi pa kwenda, kwa walimwengu, pa huruma?
Niwe ni kupanda, daraja yangu, pasi vuma,
Pasiwe ba chonda, ajae kwangu, kwa dawama.

Upi wa kudanda, kwa walimwengu, pasi kwima?
Na kuvuta nyanda, ziso wezangu, ‘pite wima,
Kwa kurandaranda, niwape dungu, wawe nyuma.

Lipi la kushinda, kwa walimwengu, kiwe chuma?
Bila ya kuponda, kwa kilimwengu, na hikima,
Ni lau wadunda, weshe mizungu, ni kizima.

Kipi kisovunda, kwa walimwengu, cha daima?
Pasi na kukonda, kwa malimwengu, yaso wema,
Angawa ni nunda, huja kiwingu, cha nakama.

©The Kenya National Examinations Council
Contact 0724333200/ 0795491185/ 0768321553 Marking Scheme

MASWALI

(a) Taja hoja zozote **nne** ambazo mwandishi anazishughulikia katika shairi. (alama 4)

(b) Eleza sifa za kiarudhi katika ubeti wa pili. (alama 6)

(c) Andika ubeti wa nne kwa lugha ya nathari. (alama 3)

(d) Kwa nini mshairi anatumia maneno; "nduzangu" na "yaso" (alama 2)

(e) Kwa nini mwandishi anauliza swali katika mwanzo wa kila ubeti? (alama 2)

(f) Eleza maana ya maneno yanayofuata kama yanavyotumika katika shairi: (alama 3)

(i) Inda

(ii) Nyonda

(iii) Mizungu

SEHEMU B: RIWAYA

NGUU ZA JADI

Jibu swali la 2 au 3

2. Eleza umuhimu wa mandhari ya majaani ukirejelea riwaya ya nguu za jadi (al. 20)

3. Fafanua jinsi wahusika mbalimbali wamedhihirisha mapenzi katika riwaya ya Nguu za Jadi. (al.20)

SEHEMU C. TAMTHILIA

T. Arege: Bembea ya Maisha

Jibu swali la 4 au la 5

4. Bembea ya Maisha ni tamthilia inayohimiza mshikamano wa kijamii. Jadili. (alama 20)

Au

5. ***Soma dondoo hili na ujibu maswali.***

"Mtu anaishi na wanawe ambao wiki nzima anawaona wakiwa usingizini; wamelala fofofo.. .Nyumba ni ya yaya."

i. Weka maneno haya kwenye muktadha wake. (alama 4)

ii. Fafanua maudhui yanayojitokeza kwenye dondoo. (alama 2)

iii. Fafanua manufaa saba ya mazingira ya dondoo hili. (alama 14)

©The Kenya National Examinations Council
Contact 0724333200/ 0795491185/ 0768321553 Marking Scheme

SEHEMU YA D

Hadithi Fupi – Mapambazuko Ya Machweo Na Hadithi Nyingine – Dw Lutomia

Jibu swali la 6 au la 7

6. Huku ukitolea mifano mwafaka ,eleza jinsi amabavyo Haki Za Watoto/Vijana zimekiukwa katika hadithi ya mapambazuko ya machweo (alama 20)

7. "...iwapo penzi hili litatia doa, basi nirudishie mfuko huu kama ishara ya kulitupa penzi langu kama)ongoo na mti wake...

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) Fafanua mbinu mbili ambazo zimetumika katika dondoo hili. (alama 4)

c) Eleza sifa sita za msemaji wa maneno haya. (alama 6)

d) EIeza umuhimu wa msemewa wa hadithi hii katika kujenga ploti. (alam 6)

Sehemu ya E
Fasihi simulizi

8. ***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali***

"Mwanangu, dunia haitaki papara. Ikiwa unataka kufanikiwa katika mustakabali wako kuwa mtoto mtiifu na mwongofu. Kumbuka kuwa asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu…"

a) Tambua na ueleze kipera hiki cha fasihi (alama 2)
b) Eleza sifa tatu za kipera hiki. (alama 3)
c) Fafanua dhima tano za kipera hiki katika jamii. (alama5)
ii) Fanani anawezaje kuihusisha hadhira katika usimulizi wake? (alama 4)

iii) Eleza utaratibu unaofuatwa wakati wa kutega na kutegua vitendawili. (alama 6)

©The Kenya National Examinations Council
Contact 0724333200/ 0795491185/ 0768321553 Marking Scheme